



JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA

TUME YA HAKI ZA BINADAMU
NA UTAWALA BORA



Juni 13,2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuongeza Uelewa kuhusu Ualbino

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau wa utetezi wa haki za Watu Wenye Ualbino duniani kote katika kuadhimisha **Siku ya Kimataifa ya Kuongeza Uelewa Kuhusu Ualbino**. Siku hii ni ya kipekee kwetu sote kwa kuwa inatukumbusha umuhimu kwa Serikali, Asasi za Kiraia, taasisi za dini na wadau wengine kutoa elimu kwa umma kuhusu ualbino na haki za Watu Wenye Ualbino. Kauli mbiu ya mwaka huu ni: **“Kuelekea sensa ya watu na makazi, tuimarishe upatikanaji wa takwimu bora kwa maisha bora. Watu Wenye Ualbino tujitokeze kuhesabiwa.”**

Kauli mbiu hii ni muhimu kwa sababu takwimu sahihi ya watu na makazi itawezesha Serikali kupanga mipango yake kwa usahihi na kufikia malengo ya kitaifa pamoja na kutambua makundi mbalimbali, ikiwemo Watu Wenye Ualbino. Kauli mbiu hii pia inaenda sambamba na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu inayoelekeza uwepo wa kanzi data ya watu wenye ulemavu.

THBUB inatambua jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wadau mbalimbali wa haki za binadamu katika kuongeza uelewa kuhusu ualbino na haki za Watu Wenye Ualbino. Pamoja na jitihada hizo, THBUB imebaini uwepo wa vitendo ambavyo ni kinyume na haki za binadamu na utu wa mtu dhidi ya Watu Wenye Ualbino.

Vitendo hivyo vinapaswa kupingwa na kulaaniwa na kila mmoja wetu. Kutokana na changamoto hizo, THBUB inapendekeza yafuatayo:

- i) Serikali kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya utetezi wa haki za binadamu kuendelea kutoa elimu kuhusu ualbino na haki za watu wenye ualbino;
- ii) Kupitia zoezi la Sensa ya watu na makazi, Serikali iwatambue Watu Wenye Ualbino na kuweka mikakati endelevu ya kuendelea kuwatambua kwenye maeneo yao;
- iii) Serikali za mitaa na vijiji zifuatilie ili kubaini vitendo vya uvunjifu wa haki za Watu Wenye Ualbino katika maeneo yao;
- iv) Jeshi la Polisi lihakikishe kuwa watuhumiwa wa vitendo vya ukatili dhidi ya Watu Wenye Ualbino wanapatikana na kufikishwa mahakamani;
- v) Wananchi watoe taarifa katika mamlaka husika juu ya vitendo vya kikatili, udhalilishaji na unyanyasaji dhidi ya Watu Wenye Ualbino katika maeneo yao; na
- vi) Wananchi waachane na imani, mila, desturi na mitazamo potofu ambayo huwafanya Watu Wenye Ualbino kujiona hawakubaliki, hawawezi na hawana mchango kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mwisho, THBUB itaendelea kushirikiana na wadau wote katika kuhakikisha haki za Watu Wenye Ualbino zinalindwa, zinakuzwa na kutetewa nchini.

Imetolewa na:



Mohamed Khamis Hamad
Makamu Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Juni 13, 2022

